

Kuisikiliza Sauti Yake.

“Kondoo wangu waisikia sauti yangu, name nawajua, nao wanifuata. Nami nawapa uzima wa Milele, wala hawatapotea, wala hawatapotea kamwe. Wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu. Baba yangu aliyenipa hao niu mkuu kuliko wote wala hakuna mtu awezaye kuwapokonya katika mkono wangu. Baba yangu.” (Yohana Mt. 10:27-29)

Hebu tukumbuke hili tunaposafiri kwenda nyumbani kwetu. Kamwe usiuache huu ujumbe ufe kutoka moyoni mwenu. Chochote ufanyacho usikubali hilo lifanyike. Utafakari juu yake usiku na mchana. Na uombe usiku na mchana ili Mungu ainue mashahidi wake sasa. Tuko tayari, kwa maana ninaamini sio muda mrefu ujao wakati utakuwa umekwisha. (**Ufunuo 10:5 -7**)

“Utakuwa ni wakati gani, ndugu Branham?” Sijui pengine leo inawezekana ikawa kesho. Kama siyo leo, nitakuwa nikiitarajia hiyo kesho. Na inaweza ikawa mwaka huu au mwaka ujao, miaka kumi pengine miaka thelathini, sijui itakuwa lini, lakini nasema kuanzia sasa na kuendelea, uwe aliye tayari kila dakika. Na sasa usilichukulie kama jambo fulani la kawaida tu. Usifanye hivyo, usipumzike mchana au usiku mpaka umezungumza na Mungu. Jiweke mbali na Uzushi. Usijichafue katika misisimko, usifanye hivyo. Hiyo ndiyo inayoleta watu wakupe lawama na unawafanya watu waliogope hilo, Ni kwa sababu ya uzushi na kupenda lawama. Usilikubali hilo hata kidogo, ukae hapo mpaka umezungumza na Mungu. Ni kwa ajili ya nafsi yako ni wewe utakayeenda kuishi milele huko ng'ambo. Uwe na uhakika kuwa siyo kupeana tu mikono na kusema kanuni au kukubali kitu fulani kwa Imani. Usifanye hivyo. Uzungumze na Mungu, na umwache Mungu azungumze na wewe (**Matayo 6:6**) na uangalie kile kinachotokea kwako. Angalia shauku zako na kile kinachotokea, hapo sasa utajua kama unazungumza na Mungu au hapana [1]

Na unaweza kuwa na uhakika. Huwezi ukawa na uhakika na Neno la Mungu kama unalisoma tu, Mungu inabidi azungumze na wewe kupitia Neno. Nuhu alikuwa na uhakika tu kwamba itaenda kunyesha mvua kama alivyoweza kuwa. Alikuwa na uhakika na hilo. Hakuna sauti zisizo na uhakika kama Mungu amesema. “Nuhu tengeneza Safina ili uweze kuikoa nyumba yako. (**Mwanzo 6;8-22**) Hiyo haikuwa sauti isiyo na uhakika. Ilionekana karma sauti isiyo na uhakika kwa watu, wakati mtu wa porini, mkulima alipopata wazo la kijinga katika kichwa chake, kwamba anakwenda kujenga Safina, na kamwe haijawahi kunyesha mvua au umande haujawahi kushuka kutoka mbiguni au chochote. “Kama hiyo sauti ya Mungu iliyosema inakuja. Mungu anao uwezo wa kuiweka pale iangukie chini. Alikuwa na uhakika inaenda kunyesha, kwasababu Neno la Mungu limesema hivyo na ilikuwa ni hakika na alijua ilikuwa ni hakika [2]

Nabii alisema juu ya ujumbe wake;

Na halafu kama kuna swali lolote ambalo hulielewi, nakuomba uchukue vitabu vyako, na halafu nyinyi mlilo na hivi vinasa sauti mnaweza kupata kanda na kuziweka nyumbani mwenu, na ukae chini na moyo uliofunguliwa. Viweke chini useme Bwana nimetulia sasa, ninaenda kusikiliza “na sasa ukinasa kitu fulani zima hiyo kanda na uende uchukue maandiko. Na Biblia ilisema Yesu alisema hayo ndiyo ambayo yananishuhudia mimi” (**Yohana Mt. 5:39**) Unaona? Na hebu tuangalie kupitia maandiko na tuone kama ni sawasawa [3]

” Kondoo waisikia sauti yangu (ambayo ni Neno) mgeni hawatamfuata (**Yohana 10:1 - 6**) Sauti yake ni nini? Sauti ya mtu yeyote ni neno lake na hii ndiyo Biblia. Lisiongezwe hata Neno moja au lisipunguzwe, kaa nayo tu hiyo sauti (**Ufunuo 22: 18 – 19**) Mgeni hawatamfuata “Dhehebu” [4]

Ndugu na Dada, hii ni saa na wakati wa kuwaita watu watoke Babiloni(**Ufunuo:18:1 - 5**). Nuru ya wakati wa jioni iko hapa(**Zakaria 14:6 - 7**). Tembeeni nuruni maadam Nuru ipo pamoja nanyi(Yohana 12: 35 - 36) Angalia waaminio waliona Neno likidhihirishwa na wakaliadini hilo. Yesu alisema, “ Kondoo wangu wanaijua sauti yangu, Neno langu, Ishara zangu za wakati Yule wa Uongo hawatamfuata” (**Yohana Mt. 10: 27 – 29**)

Roho Mtakatifu anakutaka wewe Uishi kitakatifu kila siku, katika juma na kila Usiku, ulijitenge mwenyewe na vitu vya Dunia. Lakini kanisa halitaki hivyo. Wanataka mtu wa kuwatafsiria Biblia vile wanavyotaka kuisikia hiyo. Hawatataka kusikia sauti ya Roho Mtakatifu ikizungumza kupitia Biblia. [6]

Angalia kelele nyingi,lakini hazikuvuta usikivu wa Nabii(Eliya). Nabii hakujali zile kelele nyingi. Lakini alipoisikia sauti ile ndogo ya utulivu alijua hilo ni Neno. Lakini alijifunika uso wake na akaja nje kutembea. (**1. Wafalme 19:9 – 18**) [7]

Yesu Kristo alisema siku moja, “Msipokula nyama ya Mwana Adamu na kuinywa Damu yake, hamna Uzima ndani yenu” (**Yohana 6: 53 – 69**) hakulieleza hilo

Wale mitume na wale wa siku ile ambao walikusudiwa Uzima, aliwajua hao. Alisema wote alionipa Baba watanijia (**Yohana 6:37, 44**) Jambo moja alichosema afanye ni kuifanya sauti yake ijulikane; wanaijua hiyo. Kwa maana kondoo wangu wanaijua sauti yangu “Na sauti ni Neno likielezwa.....Waliamini hiyo, hawahitaji kuithibitisha kisayansi kitu chochote, au kumuuliza Sedekayo au farisayo au yeyote yule juu ya hilo.” Nimelisema hilo wanaliadini kwa maana kondoo wanaisikia sauti yangu Na hii Biblia ni sauti ya Mungu katika maandishi, kwa sababu huu ni ufunuo wote mkamilifu wa Yesu Kristo. Agano la kale na Jipya vikiwekwa pamoja. Amina tuko hapo. [8]

“Kondoo wangu wanaisikia sauti yangu wanaijua Neno. Ni nini Sauti yake? Hii hapa. Hawawezi kufuata kanuni, lakini wao wanaisikia sauti yangu. Nao wanaifuata hiyo. [9]

Nataka nikuambie wewe sauti ni nini? Sauti ni Ishara ya Kiroho. Alimwambia Mussa”kama hawataisikia sauti ya Ishara ya kwanza wataisikia sauti ya Ishara ya pili.(Kutoka 4:1 – 9) kondoo wangu wanaisikia/wanaijua sauti yangu.

Ni lini mambo haya yanapaswa kutokea, ni siku za mwisho, Kondoo wa Mungu wataitambua hiyo, unaona, unaona ? wanaitambua hiyo ”Kondoo wangu wanaitambua mimi. Mgeni hawatamfuata.” Hawatawafuata hao wageni, Ni lazima iwe ni Ishara iliyothibitishwa kwa ajili ya siku hiyo nao wanaona hiyo. [10]

Sasa tunaona katika Waebrania sura ya 12 na mstari wa 24, kwamba lile agano jipya, ile damu inazungumza mambo mazuri. Ile damu inazungumza. Haleluya. Hiyo ndio inayoifanya iwe sahihi na au makosani. Lile Neno linatambulishwa na sauti ya ile damu. Ile sauti ya damu ni Roho Mtakatifu, ambaye analeta Uhai. Ni uhai na inaleta uhai katika Neno na kulihuisha hilo. Amen, Amen, Amen.

Hakika ile damu inazungumza. Inazungumzia mambo mazuri. Lile Agano la kale, ile damu ilizungumzia hatia, katika Agano jipya, inazungumzia ukombozi. Katika agano la kale ilizungumzia kifo/mauti na hukumu. Katika Agano jipya inazungumzia ufufuo na Uzima. Inazungumzia uponyaji, inazungumzia furaha, inazungumzia nguvu, inazungumzia uzima, inazungumzia mbingu. Na damu ile ile iliyomwagwa ardhini ambayo iliita kwa ajili ya ndugu aliyekufa, au iliyokuwa akiita ndugu yake aliyemuuwa yeye (**mwanzo 4; 8 – 13**)

Damu ya Yesu Kristo inafunika dhambi zetu zote, na inazungumza Amani na ufufuo, nguvu, Uzima na uponyaji. Na Baraka zote za ukombozi zilizoacha damu ikamwagika, inazungumza kwaajili yetu. Hakika ile damu inazungumza ooh jamani. [11]

xxxxSasa kuna njia moja pekee ambayo unaweza kuokolewa.

Hiyo ni kwa Imani unaokolewa, na hiyo ni kwa neema (**Waefeso 2:8**) Neema ya Mungu inazungumza na wewe ikakuleta wewe madhabahuni. Unatafuta Baraka za Mungu. Unatafuta Neno lake, Unamtafuta Roho Mtakatifu, unatafuta upendeleo wa Mungu, kama ndivyo unaweza kufanya hivyo kwa moyo wako wote, ukausalimisha huo. Sasa usiangalie msisimko wowote angalia ukweli, ukweli utokao moyoni mwako kwa Imani. Bwana niko tayari kufanya chochote ambacho Neno lako linaniamrisha mimi nifanye. Najisalimisha mwenyewe na vyote vilivyo ndani yangu [12]

Nataka niwaambie hili, sasa kama mtaniamini na kunisikiliza, chochote kiwacho, kiko ndani ya moyo wako, chochote kile utakacho kujua haijalishi ni ugonjwa gani, mwamini Yeye sasa. Yeye atazungumza na ninyi kama mtu binafsi, naamini hilo kwa moyo wangu wote. Roho Mtakatifu ataenda kulifanya hilo kuzungumza na wewe, kukuambia kile unachohitaji. Chochote atakachokuambia kifanye hicho, kama wewe ni kiwete, Akisema inuka na utembe, wewe inuka na utembe. Kama una kensa Naye akasema sahai kuhusu hiyo kuanzia leo na kuendelea, wewe fanya hivyo uone kama haitatokea. Kama umesimama njia panda hujui ugeukie njia ipi, Yeye atakuambia chakufanya. Ataliweka moyoni mwako sasa hivi usimtilie shaka Yeye. Nenda kalifanye. Fanya vile tu anavyokuambia ufanye. Yeye atalifanya. [13]

Na sasa, Baba tunaomba kwamba utatuzungumzia kila mmoja kupitia Neno lililoandikwa, Tupe sisi kitu fulani katika mioyo yetu, ifanye safari yetu isiyumbe yumbe, Bwana na utupe ujasiri mpya. [14]

Sasa ninaomba Mungu kwamba, popote pale ambapo haya maneno ambapo yataangukia kotekote wasikilizaji wa kanda na hawa waliopo sasa, kwamba Roho Mtakatifu atamwita sasa hivi kila yule aliyechaguliwa kimbele kabla ya kuwekwa misingi ya dunia katika kitabu cha Uzima cha Mwana kondoo(**Ufunuo 13:8**) Naomba wasikie sauti ya Mungu ikizungumza leo, ni ile sauti ndogo, sauti ya utulivu, iliyo ndani ya mioyo yao ikisema “ Hii ndiyo njia, tembeeni katika hiyo” Jalia hilo Bwana naomba hilo katika jina la Yesu Kristo. [15]

nukuu za kiingereza

1. Ishara ya kweli Washindwayo kuiona(61 – 1112) Aya 295 – 297
2. Sauti zisizo na Uhakika (61 – 0415E) Aya E46.
3. Lile neno lililonenwa ndio mbegu ya Asili (62 – 0318) Uk. 6
4. Mungu wa wakati huu muovu (65 -0801M) Aya 163
5. Matukio huwekwa wazi na Unabii (65 – 0801E) Aya 89.
6. Yule mfalme aliyekataliwa (60 - 0515), Uk 15.
7. Yule Mjumbe wa jioni (63 – 01160 Aya 214.
8. Nawe hujui (65 – 08150 Aya 149 – 152.
9. Kushawishika halafu kuhusika (62 – 0610E) Uk. 28
10. Muhuri wa sita (63 – 1128E0 Kitabu cha Mihuri Uk. 428
11. Ile Ishara (63 – 1128E) Aya 167 – 168
12. Muungano usioonekana wa Bibi Arusi wa Kristo (65 – 1125) Aya 385.
13. Ile safina (55 – 0522) Aya 181 – 182
14. Kumiliki vitu vyote (62 – 0506) Aya 34.
15. Lile shitaka (63 – 0707M) Aya. 369

Amekuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Bibilia na kazi ya haraka itazunguka dunia

Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia (Ndugu Branham katika mwenendo, utaratibu na mafundisho uk724.)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili andika kwa:

Charles E. Y. Kanju,

Box 553 Korogwe - Tanga

E-mail: Chaelika@live1.com

Cellphone: 0784 704299/ 0713230098